# Washauriwa kuboresha kiwanda cha ngozi

**Na Kija Elias, Mwanga**

**HALMASHAURI** ya Wilaya Mwanga, imeshauriwa kuboresha kiwanda cha kuchakata ngozi Usangi, ili kuongeza tija katika uzalishaji na mapato ya ndani.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Diwani wa Usangi, Amir Sarumbo kwenye kikao cha kujadili bajeti ya halmashauri hiyo kwa mwaka wa 2022/23, kilichofanyika wilayani humo.

Alisema kwenye kata yake kuna kiwanda cha kuchakata mazao ya ngozi ambacho ni kidogo, ikiwa kitaboreshwa kwa kupanuliwa na kuongezwa uwezo kitachakata ngozi nyingi, mapato ya halmashauri pia yataongezeka.

Sarumbo alisema mbali na kuongeza mapato ya halmashauri hiyo, pia wafugaji na wachinjaji walioko katika wilaya hiyo watakuwa na mahali pa kupeleka ngozi zinazotokana na mifugo yao.

Alitoa ushauri kwa uongozi wa halmashauri hiyo wakati ikitafakari ushauri wa kukiboresha, uanze mchakato wa kuweka vizuizi barabarani vitakavyosaidia kupata mapato mengi yanayotokana na ngozi za nje ya wilaya.

Diwani wa Mwaniko, Baraka Maradona na wa Mgagao, Longoviro Kipuyo walisema wilaya ina vyanzo vingi vya mapato ambavyo vikisimamiwa vema ukusanyaji mapato ya ndani utavuka makadirio ya Sh bilioni 3.

Diwani wa Kileo, Kuria Msuya alitoa ushauri kwa Mkurugenzi, Mwajuma Nasombe kuunda timu itakayoainisha maeneo yenye madini ya mchanga.

Alisema asilimia 80 ya mchanga unaotumika kwenye ujenzi mkoani hapa, yanatoka wilayani hapa, hivyo endapo halmashauri itakuwa na maeneo rasmi ya uwekezaji, itaongeza mapato.

Baraza la Madiwani Januari 26 mwaka huu, lilipitisha bajeti ya ndani ya Sh bilioni 3 kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, huku jumla kuu ya makadirio kwa kipindi hicho yakiwa ni Sh bilioni 31.3.

# Kiwanda sasa chaanza kumwagilia mashamba

**Na Gift Mongi, Moshi**

**KATIKA** kukabiliana na upotevu wa maji katika kipindi cha mabadiliko ya tabianchi yaliyofanya baadhi ya maeneo kukumbwa na ukame, kiwanda cha sukari (TPC) kimeanza umwagiliaji kwa njia ya matone.

Njia hii ya umwagiliaji imeelezwa kuwa rafiki, kwani inaokoa upotevu wa maji yasiyotumika katika mmea husika hivyo hupotea bure.

Meneja wa Tume ya Umwagiliaji ya Mkoa wa Kilimanjaro, Said Ibrahim alisema juzi kuwa wameanza kutoa elimu hiyo na kuwa TPC ambaye ni mkulima mkubwa, imeanza kuitumia.

"Tunashukuru TPC kuanza kutumia teknolojia hii, kwani itawezesha kumwagilia kwa kipindi kirefu, hasa wakati huu ambapo kuna uhaba wa maji kwenye baadhi ya maeneo," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Wilaya ya Moshi, Louis Mbuya alisema njia hiyo mbali na kuwa rafiki wa mazingira, lakini itahakikisha upatikanaji miwa kwa msimu mzima wa uzalishaji.

Alisema TPC ni miongoni mwa viwanda vikubwa mkoani Kilimanjaro na kimeajiri idadi kubwa ya wafanyakazi, hivyo njia hiyo ni sahihi kwani hawatasimama uzalishaji kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Hii njia ambayo TPC imekuja nayo itawezesha shughuli kuendelea bila kuathiriwa na hali ya hewa, na pia kama kingesimama uzalishaji idadi kubwa sana ya watu wangeathirika," alisema. Naseeb Hussein mkazi wa New Land alisema teknolojia hii ni nzuri na kuwa ingefaa kutumiwa na wakulima wengine wakubwa, ili kuendelea kuhifadhi maji yasipotee bila sababu za msingi.

Alisema kwa kipindi kirefu, wakulima wengi wamekuwa wakitumia maji mengi kumwagilia, wakati mahitaji kwa mmea ni kidogo, jambo linalofanya maji kupotea bure.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi Benki ya NMB, Aikansia Muro, akizungumza na mmoja wa washindi wa droo ya mwezi ya Kampeni ya 'NMB MastaBata Kivyako Vyako' iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard na kushoto ni Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Pendo Mfuru. (Picha na Mpiga Picha Wetu).

Scanned with CamScanner

# Kiwanda cha nyama Nguru kitakavyowapa fursa wafugaji

Na Thadei Hafigwa

NI takriban miaka mitatu tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) baada ya Serikali kufikia uamuzi wa kuunganisha mifuko ya Pensheni ya PSPF, LAPF, GEPF na PPF, na kuunda mfuko mmoja kwa ajili ya watumishi wa umma, na kuufanyia marekebisho mfuko wa NSSF ili uwe mfuko wa mahsusi kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Mfuko huo ulianzishwa kwa Sheria namba 2 ya mwaka 2018, na baada ya kupitishwa na Bunge tarehe 31, Januari, 2018 na kusainiwa na Rais tarehe 8, Februari, 2018.

Utekelezaji wa sheria hiyo ulitangazwa kwenye gazeti la Serikali tarehe 1, Agosti 2018, imekuja kuondoa sintofahamu na mkanganyiko walioupata wafanyakazi wengi wanapopata ajira mpya.

Serikali ilipoazimia kuunganisha mifuko ya pensheni na kuwa mfuko mmoja, pamoja na mambo mengine imesoma alama za nyakati kutokana na kasi ya maendeleo duniani hasa ukizingatia siku za nyuma mifuko hiyo ilikuwa ikigombania wateja hali iliyosababisha kutokuwepo na afya kwa maendeleo ya watu.

Wafanyakazi wengi wanapoingia kwenye ajira mpya jamii ilishuhudia jinsi walivyokuwa wakihaha kutafuta mfuko gani wa kujiunga nao wenye manufaa na masilahi kwao ya sasa na baada ya kustaafu, kila mfuko ulikuwa ukijinadi kuwa ni bora kuliko mwingine kama msemo wa wahenga usemao 'mwamba ngoma huvutia kwake.'

Pamoja na kusimamia pensheni kwa watumishi wa umma, mfuko huo pia umejikita katika uwekezaji wa miradi mbalimbali kwa lengo la kutunisha mfuko. Miongoni mwa miradi hiyo ni Machinjio ya Nguru Hill yaliyopo kilometa chache kutoka Manispaa ya Morogoro.

Kutokana na uwekezaji huo, hivi karibuni wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), walifanya ziara ya kutembelea kiwanda cha nyama, ziara ambayo iliratibiwa na maofisa wenye dhamana ya kusimamia Mfuko huo wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma.

Mkurugenzi Mipango na Uwezekezaji wa PSSSF, Fortunatus Magambo anasema kuwa kiwanda hicho kinatarajiwa kuanza kazi Machi, mwaka huu, na kwamba baada ya kukamilika yatakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi zaidi ya 1,000 kwa siku.

Magambo anasema kuwa nyama watakuwa wakinunua ng'ombe na mbuzi kutoka kwa wafugaji na kuwanenepesha ili kufikia viwango vya kimataifa. Anasema kwa kuwa mifugo itakuwa inanunuliwa kutoka kwa watu mbalimbali wafugaji watakuwa na soko la ng'ombe la uhakika.

Kitendo cha wahariri kupitishwa kwenye hatua mbalimbali katika machinjio hayo ni kiashiria cha utawala bora uliopo kwenye menejimenti ya PSSSF, ili dhima ya wahariri ya kuelimisha na kuhabarisha umma kwa usahihi iweze kutimia kwa weledi mkubwa kama daraja kati ya serikali, wananchi na wadau wa maendeleo.

Ni taasisi chache ambazo zimekuwa na mfumo wa kuweka wazi shughuli zao kwa umma kupitia waandishi wa habari, taasisi nyingine zimekuwa na kasumba ya kuficha taarifa zao na kusababisha wananchi kukosa haki yao ya msingi za kuapata taarifa kama ilivyoanishwa katika Katiba ya nchi, ibala ya 13.

Mfuko wa PSSSF kwa mujibu wa Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama, James Mlowe anasema kuwa vyombo habari vina jukumu kubwa katika kuhakikisha jamii inatambua mchango wa mifuko ya kijamii katika kuchangia maendeleo ya taifa.



Mitambo ya kiwanda cha nyama kilichopo Nguru mkoani Morogoro.

Mhandisi katika machinjio hayo, Zuberi Makazini anasema kuwa mabwawa ya majitaka waliyoyajenga yamelenga kuyakusanya maji yanayotoka kwenye machinjio, kisha kutibiwa kabla ya kutumika tena kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

Anasema wanatarajia kuajiri wafanyakazi zaidi ya 300, lakini kwa kuanzia watatoa ajira 120 za moja kwa moja, na kwamba kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha kazi nyingine.

Hivyo mradi huo utachangia kupunguza tatizo la ajira hususan kwa vijana wanaomaliza elimu katika ngazi mbalimbali wanaoongezeka kila mwaka, ambao wanashauku kubwa ya kutafuta ajira halali.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa TEF, Salim Said Salim ambaye ni mwanahabari mkongwe anasema ameridhishwa na mfumo wanaotumia menejimenti ya Mfuko wa PSSSF kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ikiwemo kiwanda hicho nyama cha Nguru.

"Sisi waandishi wa habari kwa kadri ya maelezo tuliyopewa na wataalam hapa, na tumeshuhudia kwa kuona kwamba uwekezaji uliofanywa katika kiwanda cha Nguru ni mkubwa, hivyo ni dhahiri kuwa PSSSF na washirika wake wamefanya kazi kubwa," anasema Salim.

Anasema kiwanda hicho kitatoa ajira za muda mfupi na mrefu na kwamba wahariri wana jukumu la kuelimisha umma na wanachama wa PSSSF juu ya umuhimu wa uwekezaji huo kwa taifa na maisha ya mtu mmoja mmoja.

Hata hivyo, pamoja na jitihada zilizofanywa na mfuko wa PSSSF katika uwekezaji mbalimbali ukiwemo ujenzi wa majengo kuelekea uchumi wa viwanda, wadau wa mfuko huo wamekuwa wakionesha kutoridhishwa na kikokotoo cha mafao kwa wastaafu hali inayoibua sintofahamu na kuiomba Serikali kuangalia upya kikotoo kicho.

Mfuko wa PSSSF moja ya chanzo chake cha mapato ni michango ya wanachama wake inayokatwa kila mwezi, hivyo wanachama wanapofika muda wa kustaafu hutegemea kupata mafao yao kutokana na utumishi wao.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama wa PSSF, James Mlowe anasema kupitia uwekezaji unafanywa na mfuko huo ni moja ya mkakati wa kuhakikisha wateja wao wanaandaliwa mazingira mazuri ya kupata stahiki zao bila ya urasimu, kwamba michango yao ipo salama.

Scanned with CamScanner



Donatus Richard. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NIPASHE UK 19.

# Sita wauawa mapigano ya wakulima, wafugaji

**Na Hamida Kamchalla,**

KILINDI

WATU sita wameuawa katika mapigano ya wakulima na wafugaji kwenye vijiji viwili mikoa ya Tanga na Manyara.

Hadi kufikia jana mchana, watu sita walikuwa wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa vibaya kwa silaha za jadi katika kijiji cha Kibirashi kilichoko Wilaya ya Kilindi (Tanga) na Kijiji cha Elerai Wilaya ya Kiteto (Manyara).

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, chanzo cha mauaji hayo ni wafugaji wa Kijiji cha Elerai kuvamia Kijiji cha Kibirishi na kuanza kuwashambulia wakulima kwa risasi na baadaye kutumia mapanga.

Alisema watu hao waligundulika kuuawa na miili yao kutelekezwa, Januari 30 mwaka huu.

"Ni kweli hayo mauaji yametokea. Kuna familia moja ya wafugaji wakiwa ndani ya boma, walivamiwa na kijana wa miaka 25, walimpiga risasi tumboni na begani.

"Baada ya tukio hilo, pakazuka taharuki kwa jamii ya wafugaji, wakidhani wamevamiwa kutokana na mgogoro wao ulioko na Kijiji cha Kibirashi.

"Kutokana na hali hiyo, yakaanza matukio yaliyosababisha wafugaji wa kuua wakulima watatu, lakini wakulima nao, wakaanza kushambulia wakawaua wafugaji watatu. Kwa hiyo waliofariki ni sita hadi sasa."

Kwa mujibu wa kamanda huyo, waliopoteza maisha ni mwanamke mmoja, wavulana wanne na mtoto wa miaka saba.

Kutokana na mauaji hayo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, alisema waliotekeleza mauaji hayo watakamatwa wakiwa hai au wafu.

Scanned with CamScanner